Hon. Antony Theuri: Asante sana, Bwana Spika. Hata mimi leo niruhusu niongee kwa Kiswahili hata kama sijiamini sana. La muhimu ni kuhakikisha ya kwamba ujumbe umewafikia. Kwanza, niwakaribishe wageni wetu walioko kwa jukwaa. Kwa minajili ya kujitabulisha, ninaitwa Antony Theuri Wambui na nawakilisha watu watukufu wa Wadi ya Nanyuki.

Nashukuru ndugu yangu Mheshimiwa Salim kwa sababu ya mjadala wa leo na niseme ya kwamba ameruka mbele. Mimi nilikuwa najipanga chinichini lakini ni vizuri kama tungeruhusiwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

tuseme kwa lugha ya Kichina ambapo tungekuwa nyumbani ningesema "*kuringa ikiuma ikiuma irima"* na hiyo tutatafsiri tukitoka kwa hili Bunge.

La muhimu niseme ya kwamba mambo ya BATUK ni mambo ambayo na kero kubwa. Wakati naongea hivi nasikia bado ile damu ya Mau Mau ndani yangu nasikia kuzizimuka. Nashukuru kwa hizi Bunge haziwezi ruhusu tuingie kwa mikuku wala rungu kwa sababu inaumiza sana. Asubuhi ya leo Bwana Spika, kwa minajili ya haya mazungumzo yetu, tuko na shida ambayo pengine haihusiani na hili sana lakini ni ukweli, nilidhani ya kwamba wakati nilichaguliwa maisha yamebadilika. Ni kweli yalibadilika lakini tuko na shida ya maji.

Kwa wiki mbili sasa ambazo zimepita ndio nimepata kueleza *Bottom up* ni kumaanisha nini kwa sababu inabidi unaenda kuchota maji kwa karai, unaweka mtungi na kuanza hiyo hali ya *Bottom up*. Katika hiyo hali ya kuoga tu, mimi niko na kijana wangu ambaye hakuenda shule kwa sababu shule yao ilikuwa na shida ya moto ingawaje ni mbali kidogo.

Katika hali ya kujitayarisha kitambulisho changu kikaanguka na kijana wangu akaniletea na kuniambia ya kwamba mimi ni mzee sana. Nilinyamaza kwa sababu kuna wimbo ambao ulikuwa unaibwa hapo wa kitaanzania unaosema, bwana nifunze kunyamaza. Nilipomuuliza ni kwa nini, ananiuliza hii miaka yako, ulikwa wakati wa *slave trade?*

Bwana Spika, mimi hata sijafikisha miaka themanini, ni kwa nini mtoto wangu anaona ni kama kwamba mimi ni wa rika na Methusela. Wakati nilikuwa nimekaa hapa, ni kama huyo kijana alikuwa katika roho ya Bwana kwa sababu yale mambo ambayo tunaongea hapa ni mambo ambayo ilikuwa inasumbua baba yangu, mama yangu na sasa pia katika kisasi changu ambacho ni cha nne. Yule shetani na uniruhusu niseme shetani kwa sababu wakati nilipoingia katika hili Bunge niliambiwa ya kwamba nimekingwa ingawaje sijui ni mpaka wapi.

Lakini, niruhusu nirejelee hawa BATUK ama hawa Wazungu kama shetani. Nikisema shetani kwa Kiswahili ni kitu ambacho ninapinga na haiendi na imani yangu. Ile kitu nasema ni ya kwamba, hata kabla ya kuenda wakati wa ukoloni wacha tuongee yale maneno ambayo yako leo. Wakati unazungumza maneno ya Ukoloni, huo ni ufisadi mkubwa sana ama sijui kwa Kiswahili nimesema tu unafiki.

Wakati tulikuwa na Mheshimiwa Lempaira wakati tulienda huko, ile kitu ilinishangaza ni ya kwamba tuliingia kwa vita Bwana Spika. Hata kama unaniona nikiwa mkonde namna hii, tunasema *it's not the size but the fight in the dog*. Lakini mimi si hiyo nimesema, baadaye ilibidi tupiganie watu wetu. Naona kuna watu hapa na kuna Televisheni hapa kwa hivyo waelewe hicho kiwanda au biashara ya BATUK kama ambavyo Mheshimiwa Leshuel amesema hapa wanatupa pesa kidogo.

Wanaenda wanatuambia katika kila mwaka wanatupatia milioni tano. Tukiingia katika hili Bunge, Mheshimiwa Mwaniki ambaye hayuko na wengine wako hapa watuletee Bajeti ya Laikipia ambayo haitafika bilioni tano. Hiyo bajeti yetu itaguza kila kona ya Kaunti. Ukitembea leo na ile bajeti Mheshimiwa Karuiru na Kagondu walipitisha hapa, tukienda kwangu Likii hutapata kitu ya bajeti hii.

Ukienda Nturukuma utapata akina mama wakipata watoto wanawaita Kawambui kwa sababu nimeanza kunyoosha barabara upande huo. Ukienda hospitali, leo nimechelewa hata sijapangusa viatu kwa sababu nilienda huko kukagua miradi ambayo bilioni tano inafanya. Nilishindwa hizi bilioni tano zinafanya kazi gani. Nilifanya uchunguzi na Mungu akitupa nafasi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

nitaleta hiyo ripoti hapa. Hao bado ni wakoloni na wakiingia hapa walisema hizo pesa watatuwachia. Sasa tumebaki hivyo na wao wanakula. Ile kitu wanatuwachia hapa kubwa ni maji taka iliyo hapo.

Chakula ambacho wanatumia hapa Mheshimiwa Spika, wanatoa Dubai kwa mhindi. Ukitoka hapa uende hivyo, wanasema wanaajiri watu wetu. Haidhuru! Mimi si mkabila. Mimi ni mtoto wa mama, simjui baba yangu; ningefurahi sana kama angekuwa mzungu. Maisha yangu pengine yangekuwa tofauti. Lakini shida ni hawa watu wanaoajiriwa. Wakati wananajisi watoto wetu na kuwaharibu na kufanya mambo mengine yote, wanasema kesi zote ndio maana nasema ni ushetani. Nisikize polepole, nikimalizia hii hotuba utakubaliana na mimi kuwa wao ni ibilisi lakini hatutawachapa katika jina la Yesu.

Hawa tutawanyoosha katika Katiba na katika haki yetu ya hii mchanga. Haiwezekani kuwa baba zetu wakufe wakimfukuza na sisi watunyanyase katika hali ya kiuchumi. Mheshimiwa Spika, hapa Nanyuki wakati wa Korona, Kesi ya kwanza ya Korona haikutoka Amerika, China au mahali pengine ila ilitoka hapa BATUK. Kisa cha kwanza cha mtu mweusi kufa kwa sababu ya Korona ni marehemu Oduori na apumzike mahali pema peponi ambaye alikuwa ni wa hapa Majengo.

Wakati wao huua mtu hapa na kufanya maovu yote hapa, wanasema ya kwamba kesi zote zipelekwe Ulaya lakini Ushetani uko hapa. Ikifika ni malipo hawataki kutulipa. Kama wao wanataka kulipa na kiwango cha hapa, mimi nashindwa kama hiyo si ushetani, ni nini? Shida yangu kubwa ni biashara. Unakuta ya kwamba pesa hazibaki hapa. Wanashikana na walaghai wadogo hapa kwetu na hapo ndipo nataka tuangalie kama vile Mheshimiwa Leshuel alisema.

Tusiruke mbele ya kamba ila tuangalie vizuri sana tusije pia tukawa tunatengenezea walaghai wadogo biashara. Nikiangalia watu wangu wa Kaskazini kuna wakati walilipiwa pesa kidogo na kamati lakini ninapotembea huko mimi hushangaa hizo pesa sioni. Kuna wajanja fulani ambao walikuja, wakachukua hizo pesa zote. Ukienda huko kaskazini, bado unapata wako na shida na ndio maana mtu aliwachwa bila miguu, mwingine bila macho, mwingine alikufa akalipwa lakini pesa zile haziko. Bado tutaangalia huo upande.

Kero langu ni hili Bwana Spika, kama tunataka kusimamisha haya mambo lazima hata sisi tusimame kama wanaume na wanawake ambao wako na ujasiri. Itabidi kama hii ni kufungwa ifungwe. Haiwezi kuwa kila siku tunapoongea hapa watu katika baruapepe zangu wanalia hakuna kazi. Wakienda huko hata saa hii wanapiganisha jamii ya kikuyu, Masai na Samburu. Mimi ninapoenda huko naambiwa ya kwamba Mheshimiwa Lempaira, Mheshimiwa Lekopien na Mheshimiwa Leshuel walisema Wakikuyu wasiende huko, wabaki huku sababu watapigwa.

Lakini bado nikichunguza na Mheshimiwa Leshuel, Lekopien na wengine walio hapa unakuta ya kwamba katika zile shamba za Wazungu wanalipa watu mara mbili ya ile pesa inabaki hapo. Ukikuja katika huu mji, kuna hoteli ambazo hawa wanajeshi hawawezi kutembea sababu kuna orodha pale. Unaambiwa wewe *Mjohnie, Kagondu, Salim au Lempaira.* Hawawezi kuja mahali ambapo tunakula maharagwe ndio mama mboga asisaidike. Hawawezi kuja kwetu Likii wachukue kuku kienyeji ambayo inaingia katika ile mitaro ilhali hiyo ndio kienyeji asili sababu waliambiwa huko kuna ukora na hao ndio wakora wakuu.

Hiyo naita ufisadi. Sisi kama Bunge sasa tulipewa Mheshimiwa Spika kwa sababu una hiyo nguvu ili hata sisi utupelekee huko tusikize kesi na wao. Heri nibebe Kizungu na kitabu ili tuseme ni lazima haki yetu ipatikane. Kama si hivyo, waondokee hapa sababu wanatufinya. Sitaki

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mseme kuwa mimi nina ukabila lakini ukiangalia vizuri sana, hawa watu ndio wanatuharibia uchumi. Sitaki kusikika kama mtu mjinga ama mtu ambaye hajasoma lakini huwezi niambia kuhusu shilingi ya Kenya na shilingi ya huyo mkoloni ni shilingi hamsini na vile mimi natoa jasho hapa na yake iko juu.

Ni nini walitumia? Ile kahawa yetu mzuri ndiyo wanakunywa na wale wasichana wetu wazuri. Sisemi yule ambaye niko naye kwa nyumba simpendi, nampenda sana lakini mkienda na wao watachukua wale wazuri sababu wako na pesa. Mimi naomba hili Bunge, ukitaka kuwakomboa watu wetu sasa hatutaenda kukesi kwa BATUK, hatutaenda kwa Kamishna Mkuu lakini wakuje huku chini wasikize mwananchi na tupitie sheria tuhakikishe kuwa haki imepatikana.

Mimi nimechoka na hii maneno yangu na Mheshimiwa Kagondu. Wanakuja kwangu wanapaka darasa mbili rangi na kuandika na maandishi makuu sana sijui kama anaandikia Mungu aonea akiwa mbinguni ilhali amepaka rangi ambayo haiwezi pita elfu mia mbili. Wamejenga visima lakini saa hizi tunahitaji. Nikimalizia, leo naomba Mungu na kumshukuru kwa sababu sisi wote ni Waheshimiwa, wale wangwana wako pale.

Kama tungewapatia nafasi watoe historia zao ili waseme kama mtu anataka kwenda Uingereza ama pahali pengine, kwenda Mbinguni ni rahisi kwa sababu ni kutubu, kuamini bwana na kuenda mbinguni. Saa hizi, mtu akisema anataka kuenda Uingereza itakuwa ni kero, itakuwa ni ngumu kama vile Biblia inasema ni kama ngamia iingilie katika tundu la Sindano sababu hawataki twende huko lakini wanapokuja hapa, wanakuja kutuharibia mazingira, wanatuletea magonjwa na laana.

Huu ndio wakati na itakuwa changamoto kwa Mheshimiwa Leshuel hapa. Wewe ndio tulichagua kama Mwenyekiti wa Kamati ya Utekelezaji. Maneno ambayo tunaongea hapa kila siku nimechoka. Ni heri jogoo hulia asubuhi na kuamsha watu. Mimi kama Kawambui nakuja hapa tu kusema. Huu ni wakati chochote tunachozungumza hapa kitekelezwe ili hawa watu waone tofauti.

Mtoto wangu aliniambia kuwa mimi ni mtu wa wakati wa utumwa saa hizi ndio nimeona ni ukweli sababu ule wakati walikuwa wanateswa mimi bado nateswa. Mtoto wangu hatateswa nitashindwa kwa nini nilikuja kwa hii dunia. Sisi wote mbele ya Mungu tuko sawa na kama tuko sawa ni lazima hapa tukae vizuri. Mimi nikienda kwao kama nitaenda waacha wanitese lakini nikiwa hapa lazima nipate haki yangu.

Ningeomba mwongozo wenu mimi nikiwa hapa. Mimi bado ni kijana na sitaki kuenda na damu moto zaidi lakini ningetaka haya mambo yaangaliwe kwa macho mawili na yatimizwe. Wakishindwa mimi bado ni mtoto wa Mau Mau tukiwa na wengine walio hapa. Tutachukua sheria mikononi na lazima haki ipatikane bila kujali kabila ambayo tumetoka. Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Speaker: Thank you, Hon. Theuri for a robust contribution. I did not know you have a specular language control for Swahili. Thank you. I want to give a chance to the Hon. Samuel Parleto Lekopien before going to Hon. Benson.

Hon. Parleto Lekopien: Thank you, Mr. Speaker, thank you very much Hon. Salim for tabling this motion in the House today. This country is in a Solis state for all of us and more so, for the Laikipia County. Why am I saying this? For how long should we lose lives? For how long will the Wanjiku die and no one will talk about it? For how long should we have the citizen die?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

For how long should we have the Murangari dying and no one questions yet no one gives an answer.

For how long should we go through a slow death because of the phosphorus that they throw out in our environment? How many lives have we lost from the Phosphorous? Has anyone thought or accounted for it? We have the NEMA (National Environment Management Authority) and I think it should be their task to find out how hazardous and how bad the phosphorous is and in what rate is it killing our people.

I will advise the County Government of Laikipia and especially the Committee of Agriculture, Environment and Cohesion Committee to do a visit of all these farms and just find out how hazardous that phosphorus is and how it is killing us slowly. What I am seeing here is we are all undergoing a slow death. Secondly, for how long should this country lose taxes because what is happening here is the British Army pays the money to the British farms in this country but they pay in British.

We need to involve KRA to find out if these guys have been paying taxes because it's too sorry that we are giving them a training ground, we are losing lives and at the same time we are losing money as a country and as a county.

I am sorry to say that Hon. Antony just said there was a budget of five billion shillings. Is that five Billion enough to let us die every day? Should we take the five billion and let the Wanjiku and the Wanjiru die every day? It's so sad. We need to sit down as a country, as a county and as a County Assembly of Laikipia and go deep into details. Thankfully, we have the Chair for Environment and Agriculture here. We need to sit down and draft something to make sure we pay a visit or bring those people here so that we can actually find out what is happening and at what rate are we dying.

Sometimes it's sad that you sit here thinking you are healthy, tomorrow you fall sick and you do not know the cause of your death. Eventually, you learn that you died of the phosphorus while you are happy thinking that you are living a healthy life but your neighbourhood is just a dumpsite of death.

Secondly, Mr. Speaker, when we go to those farms and people are being trained there and it is also sad to say that 90% of the people that are training there or people working on those farms are not from the county or the locality. Some are being sourced from Nairobi, Kisii and Kisumu while, the locals around those farms are not being employed. It's a double tragedy that you rate dying from the phosphorous and poverty.

The farm that is supposed to employ the locals around there are doing nothing. In terms of development, I am speaking about Sosian. Ol Maiso, Impala and a farm called Evan are one of the biggest training areas. They have no shares. They have not built schools, there are no boreholes and I think it's the high time we as the Members of the County Assembly of Laikipia go to the House of Commons and on their bill to explain to them in the UK the problems we are having and the problems they are causing us.

It is sad to think that only Kenya and especially around Nanyuki that we have the training ground for the British Soldiers the BATUK. I wonder why they don't train in their country. Could it be that they know the Phosphorous is dangerous for them and now they found a dumpsite somewhere in Africa and especially around Nanyuki that they can kill so many of them and pay

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

them 6 billion? It is sad and it's the high time we should all wake up to reality because if we don't, we will all perish.

As Hon. Anthony said that it was around Mt. Kenya when my father was a young man. They were actually forcefully taken to work with the British Army and they would do all sorts of things. They were even forced to go and arrest other Kenyans just because they were opposing them. I think it is sad that all this is happening in this country and in this time and era. My biggest question is and I think it is a question to all of us and especially people who are living around Nanyuki and further down to Isiolo. Recently, we have heard kids dying from explosives that are left all over.

We have heard our sisters, brothers and mothers being raped and humiliated by these British Army. There was a case in Samburu where most of the women around the training area were raped they had babies, the babies were fatherless and some of them were chased out of their families. There was a lot of divorce whereby if a mother gives birth to a white kid while the father is black and the mother is black, there were a lot of questions.

How did it happen? Some were raped during the training times and no one would dare talk because they are soldiers, they have the powers and to some extent, people believed that no one will ever defeat the BATUK. This County Assembly should sit down should engage the British Army and all these questions should be answered.

I still urge the Chair to please wake up to reality. That is by working hard because I am also a Member of the Agriculture Committee and the Environment. We need to wake up to reality and make sure that we save the lives of our people. The few times I have gone around Nanyuki, there are some specific clubs and places where they go. When you go there, you can see them humiliating girls and the boys just around Nanyuki and no one dares talk to them because they think they have money power.

For how long should we keep quiet and let everyone suffer here? Members and County Assembly of Laikipia, let's all wake up to reality and save the locals from this bad habit and slow deaths that everyone is going through. Thank you, I support the Motion.

Speaker: Thank you, Honourable Sammy Parleto. I want to give the floor to the Hon. Benson.

Hon. Benson Kuria: Asante sana, Mheshimiwa Spika kwa hii nafasi ambayo umeweza kunipatia kwa mdahalo wa huu mswada mkali kwa sababu ya jimbo hili letu la Laikipia. Nashukuru, Mheshimiwa Salim Edung ambaye ni mjumbe wa Segera kwa sababu ya kutafakari na kuona kilio cha wana Laikipia. Hapo tuko kwa sababu sisi ni wawakilishi wa jimbo hili letu la Laikipia. Kwa hivyo, wakati tunaponena haya mambo ya BATUK, hawa ni mabeberu.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda uniruhusu niwaite mabeberu kwa sababu wana Laikipia nikiguzia wanapitia janga baada ya mwezi wa saba. Ukiangalia upande wa Ol Maiso, Impala, Suyan, Kirimon, Posta na Labal; wakati wanafunzi wameingia mahali pale na wakati kuna mlipuko wa mabomu hukuwa akina mama wengi ambao huwa wamefunga mimba, mimba zao hutoka .

Nimeona Mheshimiwa Salim ameandika watatu wameathiriwa na BATUK. Hata wanaume kuanzia mwezi wa saba hakuna yule ambalo hufanya kazi. Hakuna chochote ambacho

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wao hufikiria mwana Laikipia. Hii ni kitu ninaongea nikiwa na machungu kwa sababu ukiangalia wakati BATUK wameingia Laikipia yetu, hakuna mtoto atapatikana mwezi wa saba au wa nane. Ni ukweli kwa sababu ule mlipuko huenda zaidi ya maili ishirini. Wale ambao wako karibu mahali pale akina mama hawapati mimba.

Hili ni jambo ambalo liko na uchungu kwa sababu ninajua ya kwamba ninaongea kama mtoto wa Mau Mau, mtoto wa Laikipia, Mwafrika wa Laikipia bila kuangalia kabila lolote lile kwa sababu sisi ni waathiriwa wa janga hili la BATUK. Ukiingia mahali pale ambapo wanakuja kuchukua *scouts* wakiingia mwezi wa saba, ni lazima yule kijana ambaye anaenda kuajiriwa mahali pale, kwa sababu labda atapewa elfu arubaini, ni lazima akubali mambo ya ushoga ili aguswe nyuma.

Hilo ni janga ambalo sisi hatubahatiki na ndiposa huu mjadala wa Mheshimiwa Salim utaweza kuunganisha jimbo hili letu na makali ambayo tunashuhudia. Sanasana, nasikia maneno ya mapenzi ya kibeberu wakikula *cocaine* wapatane na msichana mrembo hawataki maneno ya mbele, ni nyuma. Ni watu ambao wametuathiri na kuna faida ambayo sisi wana Laikipia tunabahatika kutoka kwao.

Mheshimiwa Spika, ningeomba ukituongoza kama baba wa Bunge hili tuwe na kikao na mama wa Kaunti ambaye ni Jane Kagiri, Gavana wetu Joshua Irungu, Seneta John Kinyua, Wabunge watatu Wachira Karani, Mwangi Kiunjuri na Sarah Lekorere halafu uchague Waheshimiwa hapa ambao wataenda kwa *Kenya Defence Forces* kupeleka makali haya. Baada ya wiki mbili ningependa Bunge hili liweze kutununulia mavazi ambayo inasema ya kwamba mikakati kama haitafanywa na hawa Beberu, Mbeberu *must go*.

Tuwe na mavazi ambayo inafanana kuonyesha ushirikiano na umoja kuonyesha mbeberu lazima aende. Ametukanyaga na ametukalia Mheshimiwa Spika. Ninajua ya kwamba kuna watu wengi wameathirika hasa Kirimon na Labal. Kuna walemavu zaidi ya mia tatu ambao wameadhirika na hawawezi kujifanyia chochote. Na wanapoingia hapa wanasema hawawezi wakalipa kodi. Sisi wenyewe kama Waheshimiwa tunalipa kodi.

Ninaomba Mheshimiwa Spika, wakati umefika Laikipia iwe ni Laikipia, wanalaikipia tusimamie sheria ya Laikipia bila matatizo na kuguswa na yeyote. Mzungu akikuja hapa, anatuona kama watu ambao hawajasoma na watu ambao ni wajinga. Kwa hivyo, nakusihi kwa sababu najua ya kwamba Biblia inasema ya kwamba tutakapo jua ukweli, ukweli utawatoa katika utumwa.

Ni jambo la kushangaza sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa naibu Spika na Mheshimiwa wa Magharibi mwa Mukogodo ambaye amechaguliwa na wananchi wa eneo lake wakienda katika pahali pale, wanaambiwa hawezi akaiingia na yule mtu hana kitambulisho cha Jamhuri ya Kenya; ni Visa. Hiyo ni aibu Mheshimiwa Spika. Hili jambo litakuwa nzuri na mwanalaikipia yeyote kutoka wadi kumi na tano wataanza kujivunia matunda ya mbeberu, kama kuna sheria itawekwa na ifuatwe. Asante.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Nasimama kuunga mkono mswada ambao umeletwa na Mheshimiwa Salim, ambao ni mswada wa kuhakikisha ya kwamba hawa Wazungu wanatupa heshima na kufanya kazi yao kisheria. Mimi nakumbuka ya kwamba kuna madhara mengi ambayo yamefanywa. Kuna watu wengi ambao wameumia katika Kaunti hii ya Laikipia. Ni jambo la busara kama sisi Kaunti ya Laikipia tutasimama wima na kutetea wananchi ambao walituchagua.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Wakati mimi nilijua mambo ya wanajeshi Waingereza nilikuwa mdogo. Nilikuwa nawaona na malori mengi na wakitufikia wanatutupia mikate na biskuti na tunafurahia kama watoto wakati huo. Wakati nimekuwa mtu mzima na kuingia kwenye huu mji wa Nanyuki nimekutana nao ana kwa ana. Najua kuna mambo mengi ambayo yamefanyika huko Laikipia Kaskazini na mengine yamefanyika kwenye hili eneo letu la Nanyuki. Ningetaka, kama mwakilishi wa watu wa Thingithu, yale mabaya ambayo yamefanyika yaangaliwe na wale ambao wameadhiriwa wapate haki yao.

Bwana Spika, nakumbuka kuna msichana aitwaye Agnes Wanjiru ambaye aliuawa na hao wanajeshi Waingereza na kutupwa kwenye shimo la maji taka. Aliaga dunia na alikuwa mtu ninayemjua, msichana tunayeongea naye na alikuwa mteja wangu kwenye biashara ninayofanya kwenye soko. Aliaga na kuacha mtoto mdogo sana ambaye amekuwa akitunzwa na shangazi yake. Hadi wa leo hiyo familia haijawahi pata haki. Haijawahi lipwa fidia.

Hapo ndipo mimi naona ya kwa kwamba kuna mambo tunayofaa kutengeneza ili makubaliano tutakayoweka yawe ya manufaa kwa watu ambao tunawakilisha na kuweza pia kuwasaidia wananchi wote bila mipaka. Bwana Spika, BATUK wako kwenye sehemu ya Thingithu, na najua ya kwamba ni watu wachache wamepata nafasi katika sehemu hiyo kwa sababu kumekuwa na watu wafisadi. Kama ni kuajiri mtu kwenye hiyo kambi wanafanya ufisadi kidogo na unapata kwamba watu tunaowakilisha hapa hawana nafasi. Kwa hivyo mimi nasimama nikitaka haki itendeke.

Jambo la kuhuzunisha ni kama vile nimesikia Wajumbe wakisema ya kwamba ukiwa umeathiriwa na jambo lolote kwenye sehemu yoyote BATUK wanapofanyia mazoezi yao eti unafaa kuenda Uingereza. Haya ni mambo tunayofaa kuangalia. Kama umeathirika ukiwa Kenya kesi yako ifanyiwe Kenya. Kama umeathirika ukiwa Uingereza basi kesi yako ifanywe huko Uingereza. Mimi nitawalaumu wale ambao wanakubali.

Kama ningekuwa Rais wa Jamhuri ya Kenya mwananchi wa hapa hawezi kudhulumiwa na aende kutafuta haki yake Ulaya. Hiyo sio haki. Hata waziri anayesimamia mambo ya Nchi za Kigeni na wa Masuala ya Ndani anayehusika na mambo ya majeshi anafaa kuingilia kati na kuhakikisha ya kwamba kama mtu ameumia hapa Kenya alipwe akiwa hapa Kenya, na kama huyo Mzungu ambaye amefanya madhara ameyafanya akiwa Kenya ashtakiwe akiwa Kenya. Ukifika Kenya umepata barua ya kuwa Mkenya, kwa hivyo uhukumiwe kulingana na sheria za Kenya.

Kwa hivyo mimi singetaka kuona hayo mambo kwamba kuna watu spesheli kuliko wengine. Hawa Wazungu wanavuta hewa kama mimi, wanakimbia kama mimi na wanafanya kila kitu ambacho nakifanya. Ni sura zao tu ndizo nyeupe. Ningesema kama ni rangi itabidi tupakwe ili tuheshimiwe basi tupakwe ili tufanane nao. Ikibidi tukutume wewe kwa sababu wewe ni mweupe basi ukae huko na kusema mambo yetu.

Mimi ningetaka kila mtu apewe haki yake. Tusiwe na mambo ya kusema huyu ama huyu. Nilisikia kwamba hawa Wazungu wakija hapa, wakisimamishwa kwa kufanya makosa barabarani hawezi kushikwa. Eti akishikwa akiwa makosani hayo makosa yapelekwe kwenye kambi. Huo ni ukoloni nami naweza kusema hayo ni mambo tunayofaa kuangalia.

Mimi ningesema tuangalie sheria wanayofuata wakiwa Kenya. Hilo tu. Mimi siwezi sema waende, hapana. Waende vipi? Kuna watu ambao wamesaidika na wengine ambao wameumia, kwa hivyo tunataka kuingilia hapo katikati. Kama Mzungu amekubaliwa na sheria ya Kenya basi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

aje. Sisi Kenya tuna sheria ya kimataifa na hatuwezi kusema huyu aje na huyu asije. Jambo ambalo mimi nataka ni kama kuna haki inayotafutwa itafutwe na kupewa mwenye haki.

Unajua sisi Wakenya ni wajanja na wajeuri wakati mwingine. Kama kuna watu ambao wameadhirika sisi tunaungana katika kikundi na kuenda kujipendekeza kusema tulipwe kwa niaba ya wale watu. Mimi nikipata mtu anayeenda kivyake kusema anatetea watu ili alipwe kivyake nitamcharaza viboko. Nitafanya kama alivyofanya Yesu alipoenda kanisani na kukuta watu wameifanya soko na kuwatandika viboko.

Kama mwananchi ameathirika wacha alipwe moja kwa moja. Ndiyo, ni vizuri kuwa na wanaoongoza yule mwananchi, bali pesa ikilipwa mwananchi apate asilimia mia moja ama asilimia tisini na tisa. Sio eti ukilipwa pesa, kuna watu wengine hapa wajeuri wanaolipwa asilimia fulani ya malipo na pengine hiyo asilimia ni sabini ama themanini inaenda kwa hao madalali na asilimia ishirini na tano tu ndiyo ya mtu aliyeathirika. Hapo ndipo mimi nasema lazima tuangalie kwa njia inayofaa.

Mimi najua madhara ambayo hawa Wazungu wamefanya. Pia naweza kusema mawili au matatu ambayo wamesaidia mtu mmoja au wawili, bali mtu mmoja au wawili hawawezi kusaidika na mamia waumie. Hapo ndipo mimi nasema kwamba tusiseme waende, maanake wakienda watu wengine wataumia. Pia hatusemi wakae hapa waumize watu wetu, hilo hatuwezi kubali. Tunataka kuwe na sheria itakayofuatwa. Aje hapa afanye mazoezi bali kwa njia inayofaa, ili nami pia nikiamua kuenda ng'ambo niende vizuri bila kuwekewa vikwazo.

Mimi bado sijaenda Uingereza bali najua nitaenda hivi karibuni mambo yakiendelea namna hii. Nitaenda huko kutetea na wakinizuia nitajua vile nitapenya. Sisi ni Mau Mau. Nimesikia wengine hapa wakisema sisi ni Mau Mau. Sisi tunajua kupenya kila mahali. Sisi tukienda kwao tunaitishwa visa. Sijui kama wao wakiingia wanaitishwa visa, sijui. Hilo ndilo nasema kuwa lazima serikali kuu iingilie kati na kujua wanakuja hapa kwa njia gani.

Vilevile, tujue kama wanajeshi wetu wanaenda kufanya mazoezi huko ili nao pia watupe hayo mabomu na kumwaga hiyo gesi wanayoita vile wanavyoita. Kama ni kuharibu hewa yao tuharibu. Kama wanatutengeneza nasi pia tuwatengeneze. Hapa ni nipe nikupe, ninyonye nikunyonye. Hayo ndio mambo ambayo ningetaka tuangalie...

Speaker: Order! Hon, Stephen. Hon. Anthony?

Hon. Anthony Theuri: Natoa ufafanuzi. Kama nilivyosema hapo awali, nina shida kutumia Swahili. Ningemuuliza kwa heshima kubwa Mheshimiwa Kagondu ajaribu... Waona leo tuna wageni na ni vibaya sana wakienda nyumbani na kusema Bungeni kuna kunyonyana. Tuko kwenye enzi mbaya ya LGBTQ. Ni vizuri asimame hapa na kusema nini inanyonywa na kwa nini. Ahsante sana.

Speaker: Hon. Stephen Ndiritu, you are being requested to give a clarification of the words you have used. Thank you.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Unajua mimi nimeongea vizuri sana lakini kile ambacho Mheshimiwa Anthony ameshika ni hicho cha kunyonywa. Sijui ni vipi bali nadhani ni kwa vile yeye hana miaka mingi kwa hivyo anakumbuka sana mambo ya kunyonya. Kile ambacho nimepeana ni mfano, nipe nikupe. Nimesema vizuri sana ni mfano. Niume nikuume. Huo ni mfano. Kama wameharibu nasi pia tuharibu ili tutoshane. Isiwe kwamba kuna mtu spesheli

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kuliko yule mwingine. Kwa hivyo nikisema ninyonye nikunyonye sina nia mbaya, ni mfano wa unile nikule. Huo ndio mfano ambao nimepeana na nadhani Mheshimiwa Theuri sasa anaelewa ninaposimama.

Nimesikia pia wajumbe wakisema kuwa mazingira yanaharibiwa. Kwa nini hawa Wazungu wanakuja tu kuharibu mazingira hapa? Ni lazima tujue ni mbinu gani itatumika ndio mazingira yetu yasiharibiwe na watu wachache. Saa hii najua mazingira yakiharibika mambo mengine yatajitokeza. Leo wanafanyia mazoezi Samburu. Walikuwa hapa Doldol juzi. Nimesikia Mheshimiwa amesema walibaka akina mama. Nikasikia Mheshimiwa Lekopien akiwa na uchungu, kwamba anajua familia ambapo bwana ni mweusi na mkewe ni mweusi bali mtoto ni mweupe. Hapo nimechanganyikiwa. Ama ni haya madawa yaliyo kwenye mabomu yametumika au njia nyingine imetumika ili huyo mtoto azaliwe.

Hayo ndio mambo tunayofaa kuangalia na kujua hiyo shida imetoka wapi. Kama kuna mtu aliyefanya kitendo kisichokubalika basi kutoka hapo tuingilie kati. Yaweza kuwa madawa ama kubakwa, ama hata masikizano. Watu wawili wakisikizana hata serikali haiwezi kuingilia. Ndipo mimi nataka kusema lazima tuweke sheria ambayo itamshika kwenye kila pande. Hatutaki watu wetu waumie. Tunataka vijana wetu wapate kazi. Hapa Nanyuki na Majengo vijana hawana kazi. Vijana wakienda hapo wanaambiwa sijui waandike barua, waje na cheti cha *Good Conduct,* ama sijui msimamizi yupi.

Bwana Spika, hapa kuna *cartel.* Mimi ningeuliza hili Bunge kwanza tushughulikie hiyo *cartel.* Hiyo cartel ambayo imekaa hapo tuiondoe. Kama hao Wazungu wameingia upande wa Kaskazini, wacha tuone vijana wamepata kazi huko na walipwe kwa njia ambayo inafaa. Sio kulipwa kama njugu karanga, eti unatolewa hii, kesho unapewa ile imeivaa na kesho kutwa ile ambayo imeungua. Unapimiwa kama hewa. Hiyo ndiyo sisi hatuwezi kubali. Kama mtu anafanya kazi ya kulima basi alipwe kulingana na ugumu ulio kwenye hilo shamba. Sio kukaa kama tunabembelezana. Ningetaka sisi tuwe na sheria ambayo itaweza kuwalinda hawa vijana wetu kila mahali.

Mimi ningesema kama mwakilishi wa watu wa Thingithu kwa sababu hawa wanajeshi Waingereza wako hapa Thingithu, kama wameajiri watu thelathini huko Laikipia Kaskazini au Samburu au Isiolo, kwa vile ni huko nje, asilimia thelathini iwe yetu. Si wanalala hapa na kukaa hapa? Kwa hivyo mimi nataka hiyo ya nje sisi tupewe asilimia thelathini. Kama wameajiri watu mia moja, thelathini watoke kwenye wodi ya Thingithu ili tuendelee mbele. Kwa wanaoajiriwa hapa sisi tupewe asilimia sabini ndio wale wanaotoka Mukogodo Magharibi pia wapate kazi. Wanaotoka Sosian pia wapate kazi. Ukija hapa utapata kuwa wanaofanya kazi hapo hata sio watu wa Laikipia. Mimi nasema hivyo nikiwa na ushahidi wa kutosha. Hakuna mtu wa Laikipia aliye hapo isipokuwa mmoja au wawili, na wanaofanya huko labda ni kazi ya kufagia. Wanaofanya kazi kubwa ni watu wa nje waliopitia kwenye mlango wa *cartel.*

Kwa hivyo tuketi chini na kusuluhisha haya maneno. Sisi kama Bunge la Laikipia tusimame wima tutetee watu wetu na kuhakikisha ya kwamba haki imetendeka kwa kila mtu. Naomba kukomea hapo na kumshukuru Mheshimiwa Edung Salim ambaye ni jirani yangu hapa kwa huo mswada ambao ameuleta hapa wa kuhakikisha ya kwamba tumeheshimiwa na kupewa haki kama watu wa Laikipia. Tuhakikishe pia ya kwamba kama hao wanajeshi Waingereza wanafanya mazoezi hapa Laikipia tupatiwe pesa ya kutosha ya ushuru kama vile mwananchi wa kawaida anatoa. Mama mboga hapa akiuza mboga yake anaitishwa ishirini, na kesho unasikia

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ameongezewa. Wanajeshi Waingereza wakija hapa hawatoi ushuru wowote. Hawatoi chochote, ni kuwabembeleza tu wasichana wetu hapa na kuwaachia kitu kidogo.

Nimemsikia Mheshimiwa Tony akisema wanawachukua wale warembo kabisa. Sijui wanaenda nao wapi ama ni nia gani wako nayo nao, bali hata kama wanafanya wanavyofanya basi wapate faida kubwa ili kesho asirudie hicho kitendo. Wapate faida kubwa kutokana na hilo kama kunao wanalolifanya. Tunajua Kenya hakuna sheria ya kufanya hayo mambo ya kutafuta warembo, hakuna hiyo sheria. Wanaofanya hivyo wanafanya kinyume na sheria, kwa hivyo watakaopatikana wawekwe ndani. Mimi nataka Wanajeshi Waingereza wakiwa hapa walipe ushuru ili watu wa Laikipia wapate manufaa wanayostahili. Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa hii nafasi, maanake najua tunakuheshimu na unatupeleka vizuri. Ahsante.

Speaker: Thank you, Hon. Stephen Ndiritu for a robust contribution to the motion. I now want to call upon the Mover of the motion to reply. Welcome, Hon. Salim Edung.

Hon. Salim Edung: Bwana Spika, nashukuru kwa huu mswada ambao umekuwa kwenye hili Bunge. Nashukuru pia Wabunge wote wa Kaunti ambao wameunga mkono, nasema ahsante sana.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: The sittings of this House now stand adjourned until tomorrow, Thursday, 9th March 2023 at 2.30 p.m.

The House rose at 4.29 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*